**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA WAZIRI MKUU**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**MKOA WA KATAVI**

# HALMASHAURI YA WILAYA YA NSIMBO.
# MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE ZA SEKONDARI ZA SERIKALI TANZANIA MWAKA...............................

SHULE YA SEKONDARI KATAVI WASICHANA.
S.L.P 534.
**NSIMBO.**
Tarehe...................

Mzazi/ Mlezi wa Mwanafunzi

.............................................

S.L.P ................................,

...........................................

**YAH: MAELEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI YA KATAVI WASICHANA.**

Nafurahia kukutaarifu kuwa Mwanao amechaguliwa kujiunga na kidato cha tano katika Shule ya Sekondari **Katavi Wasichana** mwaka ............... Shule hii ipo umbali wa takribani km 7 kutoka Makao Makuu ya Halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo. Kwa wanafunzi watakao tokea barabara ya Tabora watashuka kituo cha mabasi Nsimbo,usafiri wa bajaji/bodaboda unapatikana kituo cha mabasi Nsimbo. kwa watakao toka barabara ya Mbeya na Kigoma watashukia stendi kuu ya Mizengo Pinda na usafiri wa bajaji/bodaboda na taxi unapatikana kwa kwenda shuleni.
Tahasusi zinazopatikana shuleni hapa ni **CBG, PCB, PCM** na **P.M.C**

Muhula wa Masomo unaanza tarehe……………, hata hivyo tarehe ya kuanza muhula itategemeana na itakavyotangazwa na serikali.

Mambo Muhimu ya Kuzingatia: -

## 2.1 Sare za Shule.

(i) Sketi tatu rangi ya "**Blue masai**". (zitapatikana shuleni ukipenda kwa shilingi 30,000@1).
(ii) Mashati Mawili meupe aina ya tomato ndefu Mikono yenye nembo ya Shule.
(iii) Kwa watakao vaa hijabu, ni Majuba mawili ya rangi nyeupe yawe marefu yafunike kifua cha Mwanafunzi, pia yawe marefu kufunika Kifundo cha Mikono akisimama yasiguse Kiuno. Pia, Majuba mawili ya rangi ya bluu Bahari kwa ajili ya kushindia.
(iv) Raba nyeusi, jezi rangi ya pinki (full kits yaani bukta na T-Shirt) wakati wa Michezo kila Mwanafunzi atalazimika kuvaa sare ya Michezo.
(v) Kiatu cheusi cha Ngozi cha kufunga na Kamba kwa ajili ya darasani pamoja na simple raba nyeusi kwa ajili ya muda wa jioni.
(vi) Soksi nyeupe jozi tatu zisizo na urembo au alama yoyote ya rangi
(vii) Sweta moja rangi ya light blue yenye nembo ya Shule.
(viii) T-Shirt tatu moja ya darasani rangi ya maziwa na mbili za kushindia ni rangi za kijivu (shamba dress), unaweza kuzipata shuleni ukipenda kwa shilingi 20,000/=@ 1.
(ix) Kandambili (isiwe yeboyebo) pea mbili.
(x) Kumbuka kuja na Kanga/ Kitenge pamoja na taulo
(xi) Mashuka jozi nne rangi ya kijani Mgomba, blanketi moja, mto na foronya moja, chandarua rangi nyeupe.
(xii) Nguo za ndani za kutosha mpya (chupi kuanzia sita na kuendelea) underskit/ shimizi, sidria 2night dress/ na Tight dress kuanzia mbili na kuendelea.
(xiii) Track Suit rangi nyeusi.

NB: Usishone sketi kuepuka usumbufu wa kushona mara mbili endapo mzazi utakosea rangi ya kitambaa.

## 2.2 Mahitaji mengine ambayo Mwanafunzi anapaswa kuja nayo Shuleni.

(i) Madaftari 12 counterbook quire 3
(ii) Ream A4 ya karatasi (2) kwa Mwaka
(iii) Godoro inchi mbili na nusu kwa sita
(iv) Vyombo vya chakula (Sahani, Bakuli, Kijiko na Kikombe).
(v) Ndoo 2 lita kumi zenye Mfuniko.
(vi) Dissecting kit kwa wanafunzi wanaosoma Biology (full kit).
(vii) Scientific calculator
(viii) Dawa ya kusafishia vyoo aina ya **Careline** Disifectant **lita 5** na lita 1 ya ARO (kwa mwaka)
(ix) Spring file kwa ajili ya kutunza kumbukumbu za Mwanafunzi

(x) Inashauriwa ununue Sanduku la kutunzia vitu.
(xi) Taa ya solar au tochi kwa ajili ya dharura endapo umeme utakatika.

**VITABU VYA KUJISOMEA**

**Mwanafunzi atanunua vitabu kulingana na tahasusi yake;**

**PHYSICS:**

a) C and S (2008) Principles of Physics for Class x11 & x12, New Delhi.
b) Nelkon & Parker (1995) Advanced Level Physics 7 edition.Longman international Education.
c) Duncan T, New Understanding Physics for A-level.

**CHEMISTRY**

a) Conceptual Chemistry – Chand S.K
b) Chemistry in action – Michael Freematle
c) Physical chemistry for A-level and Undergraduate: Mkayuba and Ddungu
d) Advanced inorganic Chemistry part I and II – TIE
e) Soil and Environmental Chemistry

**BIOLOGY**

a) Taylor, D.J (1997) Biological science, Cambridge University Press.
b) Susan Toole – Understanding Biology.

**MATHEMATICS**

a) Backhouse, Pure mathematics 1
b) Backhouse, Pure mathematics 2

**GEOGRAPHY**

a) Certificate of Geography (oxford)……….by Mary Mugo. Robert Kamugat and Paul Kibuuka
b) General Geography in diagrams…………by R.B Bunnet
c) Photography Interpretation and elementary surveying for secondary A-level.
d) Regional Geography …………by Nyangwine and Msabila.
e) Certificate of Human and Economic Geography……by Morgan.
f) Word Geographical Atlas

**GENERAL STUDIES**

a) Richard,R,F. Mbalase General study for Advanced Level Certificate.
b) Mgaywa,B,M. General study for Advanced level

C. **VIFAA VINGINE VINAVYOHITAJIKA**

Mwanafunzi anapaswa kuja na vifaa vifuatavyo: -

<u>**C.B.G.**</u>

1. <u>Jembe moja na mpini wake</u>
2. <u>Soft broom</u>
3. <u>Fagio ya chelewa</u>
4. <u>Mopper</u>

**P.C.B.**

1.Jembe Moja na mpini
2.Hard broom
3. Fagio wa chelewa
4.Mopper

**P.C.M.**

1, Squizer na ndoo yake
2.Jembe moja na mpini
3.Toilet scrubing brush
4.Mopper

**P.M.C.**

1.Fyekeo, reki na jembe
2.Squizer na ndoo yake.

**MICHANGO MBALIMBALI**

**a) Shule ya bweni**

| | |
|---|---|
| Michango ya uendeshaji wa shule | 65,000/= |
| Tahadhari | 5,000/= |
| Nembo | 5,000/= |
| Kitambulisho cha shule | 5,000/= |
| JUMLA | 80,000/= |

Michango hii iingizwe katika Benki ya CRDB kwenye account **no.0150854570600** KATAVI WASICHANA SECONDARY SCHOOL. Mwanafunzi aje na Bank pay in slip, pia mwanafunzi afunguliwe akaunti na aje na kadi yake ili fedha ya matumizi utaweka kwenye akaunti yake kuondoa usumbufu.

N.B: Mwanafunzi aje na (50,400/=) kwa ajili ya Bima na (10,000/=) kwa ajili huduma ya kwanza. Mwanafunzi pia anashauriwa kufungua account ya CRDB kwa ajili ya matumizi binafsi, hakutakuwa na huduma ya kutumiwa fedha kwa mitandao ya simu kwa walimu.

## 3. Sheria na Kanuni muhimu za Shule

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendelezaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

### 3.1 Sheria na Kanuni za Shule.

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule.
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku (Night Preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa.
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule.
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa.
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote.
ix. Kutunza mali za shule
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari na
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

MUHIMU:

- ❖ Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuelni kwa namana yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi.

- ❖ Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu.

- ❖ Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa).

3.2 Makosa yatakayosabisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na :-

i. Wizi
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa / utoro
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo.
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu / walezi na jamii kwa ujumla.
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote Yule.
vi. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni au kusuka kwa mtindo wa ususi uliokubalika na uongozi wa shule
vii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya.
viii. Uvutaji wa sigara.
ix. Uasherati, mahusiano ya jinsia moja, kuolewa.
x. Kupata ujauzito au kutoa mimba

xi. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi.
xii. kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni.
xiii. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule.
xiv. Kudharau Bendera ya Taifa.
xv. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunya sumu na
xvi. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

NB: Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgonjwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa.

*TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KWA NAMBA HII* ***0763 414 888 (Mkuu wa Shule)***

**KARIBU SANA KATIKA SHULE YA SEKONDARI KATAVI WASICHANA**

Elinesi S. Mwangomba
**MKUU WA SHULE**
**SHULE YA SEKONDARI KATAVI WASICHANA**

NAMBA ZA MAWASILIANO

1. 0767961479/0624561479 –**MAKAMU MKUU WA SHULE**
2. 0752056983 **– MTAALUMA**
3. 0767385166 - **MHASIBU**

SHULE YA SEKONDARY KATAVI
WASICHANA,
P.O.BOX 534,
**NSIMBO.**

Ref. No …………………………………… Tarehe………

PART A:

To the Medical Officer,

………………………………………
………………………………………

REF: ………………………………………………………………………………………

Please examine the above-named student as to her physical and mental fitness for being a full-time student.

The examination should include the following categories (a-d).

(i)Eyesight (ii) Hearing (iii) Speech (iv) Limbs (v) General Diseases (vi)Leprosy (vii)Epilepsy.

(viii)Neurosis (ix)Other serious diseases e.g.., Asthma, T.B., etc.

**PART B: MEDICAL CERTIFICATE**

(To be completed by a GOVERNMENT MEDICAL OFFICER)

I have examined the above-named student and confirm that she is physically fit/not fit for a full time secondary school education.

(i) Eyesight …………………………………………………
(ii) Hearing …………………………………………………
(iii) Speech ………………………………………………
(iv) General diseases ………………………………………
(v) Leprosy …………………………………………………
(vi) Epilepsy ………………………………………………
(vii) Neurosis ………………………………………………
(viii) Other serious diseases e.g. Asthma …………………
(ix) T.B. ……………………………………………………
(x) Pregnancy ……………………………………………

Comments ………………………………………………………………………………
……………………… ……………………………………………………………………

Name …………………………………date …………………… Signature ……………

STATION …………………………………… DESIGNATIO ………………………………

N.B,I request this form to be returned to the school in a sealed envelope
Fomu hii ikijazwa irudishwe mwanafunzi aje nayo anapokuja Shuleni.

# HALMASHAURI YA WILAYA YA NSIMBO
## SHULE YA SEKONDARI KATAVI WASICHANA
## FOMU YA TAARIFA BINAFSI YA MWANFUNZI, KUKUBALI SHERIA ZA SHULE NA NAFASI YA SHULE ALIYOPEWA.

PASSPORT

YA

KARIBUNI

### A. TAARIFA BINAFSI YA MWANAFUNZI

1. JINA LA MWANAFUNZI:- ……………………………………….
2. TAREHE YA KUZALIWA:- ……………………………………..
3. MAHALI ALIPOZALIWA:- MKOA …………………. WILAYA …………….
   KIJIJI ……………………………
   ANAPOISHI KWA SASA:
   MKOA ……………………. WILAYA ………………. KIJIJI ………………..
4. URAIA:- MTANZANIA/ SIYO MTANZANI:- ………………………
   KABILA …………………………….
5. DINI/DHEHEBU:-
   ………………………………………………………………………………
6. SHULE ALIYOTOKA: ……………………………….
7. SHULE NILIYOFANYIA MTIHANI WA DARASA LA SABA ……………….
   WILAYA ………………………….. MKOA ……………………………………

**B KUKUBALI NAFASI NA MAELEKEZO ULIYOPEWA.**

MIMI ………………………………. KIDATO CHA ……………. MWAKA …………… Nimesoma na kuyaelewa maelekezo yote. Hivyo nakubali kuipokea nafasi niliyopewa. Nathibitisha kwamba nimekubali kujiunga na shule hii kwa hiari na nimepokea maagizo na maelekezo bila kulazimishwa na naahidi kuyazingatia na kutimiza yale ninayopaswa kutimiza bila kulazimishwa. Nitasoma kwa bidii ili nifaulu mitihani yote ya ndani na nje.

**TAREHE …………………………..** **SAINI: ……………………………….**

### B. KUKUBALI SHERIA ZA SHULE MWANAFUNZI

Mimi: -………………………………………………………………………………… nimezisoma na kuzielewa sharia, taratibu, kanuni na miongozo ya shule iliyomo kwenye fomu hii na nitakayosomewa wakti wa Orientation course. Ninaahidi kwamba nitazingatia na kutii masharti, sharia, kanuni, taratibu, miongozo ya shule na maelekezo mengine nitakayopewa na walimu, watumishi wasio walimu na viongozi wote wa shule. Sitashiriki katika mgomo, fujo, wala makosa ya jinai yaliyoorodheshwa hapo juu. Nikivunuja au kukiuka maelekezo

na sharia yoyote niko tayari kuwajibishwa kulingana na adhabu zilizoorodheshwa kwa kila kosa.

**TAREHE …………………………………… SAINI ………………………………………**

**C. TAARIFA YA MZAZI / MLEZI: (ANDIKA MAJINA MATATU)**

1. JINA LA BABA …………………………………. MAHALI ANAPOISHI:…….
   YUKO HAI / AMEFARIKI ……………………………KAZI YA BABA ………
   SIMU YA BABA ……………………. S.L.P ……………MJI………………….
2. JINA LA MAMA ……………………………….
   MAHALI ANAPOISHI ………………………… YUKO HAI/
   AMEFARIKI ………………………… KAZI YA
   MAMA ………………………… SIMU YA MAMA …………………….
   S.L.P ……………… MJI ……………………….

**ENDAPO MWANAFUZNI ANALELEWA NA MLEZI:-**

3. JINA LA MLEZI WA KIUME ……………………………………………
   MAHALI ANAPOISHI ……………………………….
   UHUSIANO ……………………………………………
   SIMU: …………………………………………………….
   S.L.P …………………… MJI …………………………

4. JINA LA MLEZI WA KIKE ………………………………………………..
   MAHALI ANAPOISHI …………………………………..
   UHUSIANO ………………………………………………
   SIMU ……………………………………………………..
   S.L.P ………………………… MJI …………………….

**D. MZAZI / MLEZI (AJAZE SEHEMU HII):**

Mimi ………………………………………… nikiwa Mzazi / Mlezi nimezisoma sheria na maagizo mengine ya shule yanayomhusu mwanfunzi ………………………………………………na ninaahidi kutimiza wajibu wangu kama Mzazi/Mlezi wa mtoto huyu kwa: kumshauri ipasavyo ili awe mwanafunzi mwenye nidhamu na ufaulu mzuri.

Pia naahidi kumtimizia mahitaji yake ya shule.

Nitahudhuria vikao vya shule kwa kadri vitakavyokuwa vinaitishwa na endapo sitahudhuria nitakubaliana na maamuzi yatakayokuwa yametolewa na nitawajibikika kulingana na maamuzi hayo.

**TAREHE:-………………………………. SAINI ……………………………….**

**E. SEHEMU YA NDUGU WA KARIBU**

Ndugu wa karibu watatu (3) wanaoruhusiwa kumtembelea mwanafunzi.
Majina Matatu Mfano: JUMA MUSA HASANI.

| | JINA | UHUSIANO | NAMBA ZA SIMU |
|---|---|---|---|
| 1. | ....................................... | ......................... | ......................... |
| 2. | ....................................... | ......................... | ......................... |